Jina ........................................................................................................ Nambari..............................................

102/2 Sahihi ..................................................

Tarehe ..................................................

**KISWAHILI**
Karatasi ya Pili
(Ufahamu, ufupisho, Sarufi na matumizi ya lugha na Isimujamii)
**Julai / Agosti 2016**

Muda: Saa 2½

# TATHMINI YA PAMOJA YA KAUNTI NDOGO YA KERICHO MAGHARIBI

Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya

**Kidato cha Nne**

## KISWAHILI

Karatasi - 102/2

**Julai / Agosti 2016**

**Muda :** Saa 2½

for more free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or Call: 0720502479

## MAAGIZO

- Andika jina na nambari yako kwenye nafasi ulizoachiwa hapo juu.
- Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani.
- Jibu maswali yote.
- Andika majibu yako katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.
- Majibu yako yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| **JUMLA** | **80** | |

1. UFAHAMU (alama 15)

Soma taarifa inayofuata kisha uyajibu maswali

Kibwana Jaku - ndilo jina walilompa wazee wake; lakini jina lake analoitwa sasa ni Farouk Hilal. Mwenyewe halitambui jina la Kibwana, kwani alichukuliwa kwenye utamu wa mapenzi ya wazazi wake alipokuwa bado ananyonya ziwa la mamake.

Bipole alimtoa mwanawe shingo upande na chozi kifua tele. Afanye nini? Mtoto mmoja alikuwa mzigo kwake, seuze wawili. Masikini mama-mtu hakujua furaha ya mwanawe, na moyo wake daima ulijaa simango, Baada ya kwisha chukuliwa mwanawe, popote alipomwona mama mjamzito, alikumbuka yeye alipoibeba mimba ile ya watoto pacha, akazaa watoto wawili wanaume; na mmoja akachukuliwa. Mara nyingi, alipokiona kitoto **kikibimbwa** na mamaake, yeye alifumwa na yaleiti, akajilaumu kwa nini amemgawa mwanawe Kibwana, kwa nini ametupa damu yake. Kazaa kama asiyezaa - mimba kabeba yeye, swenene kaona yeye, uchungu kavumilia yeye, lakini haki ya ulezi, mavi na mikojo, fahari ya mama, pamoja na uchangamfu wa kitoto, kilio cha ucheshi, umemwendea mtu mwengine kabisa. Ama kweli, kuzaa mwana si hoja, hoja majaaliwa. Aliikumbuka nyimbo aliyokuwa akiimba marehemu mamaake, alipokuwa akichombeza ndugu zake.

Kuzaa mwana si pato,
Pato ni kumvyeleza,
Ni kama kuota ndoto,
Ukaelekea kiza.

Walioimba wimbo huu hakika walisibu.

'Bibi we ... ' alionya Bi-wa-Minarani, 'nachukua mtoto kwa ulezi, mavi, mikojo ... usidhani najipagaza ulezi, hashakum, isiwe leo nalea, kikishachuchuka kitoto ukanijia mdomo juu unataka mwanao, tutashtakiana enn; mtoto namchukua, **usimjue bee wala - tee,** usimpitie, usimuulize, wala usitake kumuona; tiasaini,' alikazania Bi-wa -Minarani.

'Mwanangu ... ' alilia Bipole.

'Nyamaza,' alinguruma Bwana Jaku, 'mwache amchukue mtoto, mwache ende naye, utaweza kuwalisha watoto wawili we?'

Bipole hakuwa na la kufanya. Mbele ya sauti ya mumewe, yake haikunyanyuka wala haikusikika. Amri kali ya mumewe, ilimchinyang'a ini lake na ukali-moto wake ulimrejesha nyuma. Tabia ya mumewe ya kuwatenga watoto wao ilimvunjavunja. Alimwona kama paka shume anayekula wanawe. Mtoto wake mmoja, Pandu, aligombana na babaake, akahajiri hajuulikani alikokwendea; mtoto mwengine, Fumu, amelazimishwa ende akatafute kazi mjini. . "

'Nenda, na kama hukupata kazi, usirejeehapa, sisi hatuwezi kulisha wajane, umeshakuwa mzigo mzito.'

Mara ngapi Bipole alitamani angalau apewe fursa aibebe hiyo mizigo aliyoshindwa kuibeba mumewe; mizigo iliyomlazimu kuibeba hata kama itamvunja mgongo. Alitamani adahadari na wanawe, akipata ale na wanawe, akikosa anywe maji na wanawe; lakini wapi, alililoliona likamuumiza ni kutengwa nao, wakiachwa watambe na ulimwengu kama nyama-mwitu.

Alilolishika Bwana Jaku ndio hilohilo, na sasa kati ya hawa watoto pacha, Kibwana anatokomezwa, kabakiwa na Bakari.

Chozi moto lilimmwaika. Alijiona kama koo la kuku lililotaga lisiyaone mayai yake yalikokwendea. Alinyang'anywa hivi hivi anaona. Alitia saini warka wa mtoto kama mtu aliyeuza shamba la minazi.

Lakini uchungu wa mwana mgumu. Baada ya miaka sita ya mateso na utengano na mwanawe, Bipole alifunga safari ya kwenda kumtafuta mwanawe kwa Bi-wa-Minarani, yule bibi mwenye chake aliyekosezwa uzazi na Mungu, akapita kukwapura wana wa wenziwe. Ati alimwendea Bipole ampe Kibwana amlee, na mchache wa haya bibi huyo, alimkaukia mwana wa mwenziwe akamnyang'anya mtoto wake kimachomacho. Bipole aliigundua kasri ya Bi-wa-Minarani; lakini afadhali asingalikwenda, alifukuzwa kama mgonjwa wa tauni. 'Una mwana wewe hapa? Warka nnao, ukitaka salama yako ukomea, la si hivyo, polisi ipo, itatuamulia sheria. Ulimtoa mtoto kwa hiari yako ati,' alipayukwa Bi-wa-Minarani.

'Anga ... angalau nimwone bibiye, he, bibiangu uchungu wa mwana mgumu, huujui nini? Angalau nimwo . . .' Bipole alilia akaomba na kuangukia, lakini alisukumwa nje na kufungiwa mlango. Alijizoazoa, akainuka; kaemewa, mzito wa majonzi, jitimai na uchungu juu ya uchungu. Alinyanyua

for more free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or Call: 0720502479

nikono juu.

'Kama damu ya mtu inapotea . . . kama ile ni damu yangu, Mungu atanihukumia, atanionyesha hapa hapa duniani. Ati sheria, sheria kama niloiba cha mtu; sheria mbele ya damu yangu mwenyewe, miezi kisa?'

Maswali

a) Ipe taarifa hii anwani mwafaka. (alama 1)

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

b) Eleza sababu za Farouk Hilal kutojua jina lake asili (alama 2)

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

c) Eleza jinsi Bipole anavyoathiriwa kwa kumtoa mwanawe. (alama 3)

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

d) Taja sababu **tatu** zilizomfanya Bi. Pole kumtoa mwanawe. (alama 3)

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

e) Eleza sifa **nne** za Bw. Jaku (alama 4)

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

f) Eleza maana ya vifungu vifuatavyo (alama 2)

i) Usimjue be wala te ..................................................................................................

..................................................................................................................................

ii) Alijiona kama koo la kuku lililotaga lisiyaone mayai yake yalikokwendea

..................................................................................................................................

for more free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or Call: 0720502479

**2. UFUPISHO (alama 15)**

Soma taarifa hii kisha ujibu maswali yanayofuata.

Uchumi wa Afrika Mashariki kwa kiasi kikubwa unategemea sana kilimo ambacho kimeajiri karibu asilimia 80 ya wakazi wake. Hata hivyo pamoja na kuajiri wananchi wengi kilimo bado kinachangia kidogo katika Pato la Mataifa ya Afrika Mashariki. Kulingana na takwimu za mwaka 2014, kilimo kilichangia kwa asilimia 23 katika pato la nchi hizi na takriban asilimia 30 katika mauzo ya nje.

Wingi na ubora wa mazao yanayozalishwa unaashiria fursa ya kufanya biashara ya tija. Aidha kukua kwa soko la mazao kunakotokana na kuongezeka kwa kasi kwa idadi ya watu duniani kunaashiria kuongezeka kwa mahitaji ya chakula na kuuza katika masoko ya nje. Kwa kutambua umuhimu wa fursa hizo,

Taasisi ya Utafiti wa Kiuchumi na Kijamii (ESRF) iliendesha mafunzo kwa wananchi kuhusu fursa mpya katika kilimo biashara. Katika mafunzo hayo washiriki walielimishwa kuhusu shamba kitalu, kilimo bila kutumia udongo, ujasiriamali, ufugaji samaki katika mabwawa, matanki na vizimba, chakula cha mifugo na mbolea na ufugaji bora wa kuku.

Mkurugenzi wa ESRF, Dk. Tausi Kida, anasema kukua kwa teknolojia duniani kumeongeza fursa nyingi katika sekta mbalimbali za maendeleo ikiwano kilimo. Anasema walifanya utafiti katika maeneo mbalimbali ya Afrika Mashariki na kujifunza mengi kuhusu fursa zilizoko katika kilimo biashara.

"Teknolojia imewezesha wakulima katika sehemu mbalimbali duniani kutokutegemea tena mvua, wakulima kutumia eneo dogo la ardhi kuzalisha mazao mengi yaliyo bora, wakulima sasa wanaweza kupata taarifa mbalimbali kuhusu kilimo cha kisasa toka kwa wataalamu kwa haraka hivyo kusaidia kupata mavuno mengi na bora," anasema Dk. Kida.

Kutokana na ongezeko la watu na maendeleo ya kijamii na kiuchumi, mahitaji ya samaki yameendelea kuongezeka siku hadi siku, hivyo kusababisha uzalishaji samaki kutoka kwenye vyanzo vya asili kupungua kwa kasi. Ili kukabiliana na upungufu huu hivi sasa. Sekta binafsi inahimizwa kuingia katika ufungaji wa samaki ili kutosheleza mahitaji ya soko. Wananchi wanahamasishwa watumie teknolojia mpya ya vizimba ambayo huwezesha kuzalisha samaki wengi katika eneo dogo.

Teknolojia ya shamba kitalu (green house) ni aina ya mabanda yanayojengwa na kuzungushiwa vyandarua maalumu ambavyo husaidia kuchuja mionzi ya jua isiyofaa na kuzuia wadudu wasiingie ndani ya mimea

Mkuu wa kitengo cha ujasiriamali katika Taasisi ya Usimamizi na Maendeleo alihamasisha wakulima wutumie teknolojia hiyo ambayo ina sifa sana na pia huyafanya mazao kukua kwa haraka na kuwa na ubora unaotakiwa.

Ubora wa mazao ni changamoto kwa wakulima wengi wa Afrika Mashariki, lakini kwa kutumia teknolojia hii mkulima ana uhakika wa kutumia gharama kidogo na kuvuna mazao bora.

Maswali

a) Fupisha aya tatu za kwanza (Maneno 50 - 6) (alama 7)

**Matayarisho**

................................................................................................................................................

................................................................................................................................................

................................................................................................................................................

................................................................................................................................................

................................................................................................................................................

................................................................................................................................................

................................................................................................................................................

................................................................................................................................................

.................................................................................................................................................................

Jibu

.................................................................................................................................................................

.................................................................................................................................................................

b) Ziandike aya nne za mwisho kwa ufupi (maneno 90 (alama 9)

**Matayarisho**

.................................................................................................................................................................

.................................................................................................................................................................

.................................................................................................................................................................

for more free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or Call: 0720502479

**Jibu**

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

**3. SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA. (alama 40)**

a) Taja na utambue aina mbili za sauti ghuna za ufizi. (alama 2)

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

b) Tambua aina za silabi zinazounda neno hili (alama 2)

Muktadha

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

c) Tunga sentensi moja ukitumia -a unganifu na **na** kama vihusishi. (alama 2)

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

d) Ainisha vivumishi katika sentensi ifautayo (alama 2)

Mtoto wa jirani mwenye shamba kubwa amekutana na mama mzazi baada ya miaka.

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

..................................................................................................................................................

for more free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or Call: 0720502479

e) Andika upya sentensi ifuatayo kwa kunyambua kitenzi kilichopigiwa mstari katika kauli ya kutendesha. (alama 2)

Mama alimfanya mtoto anywe maziwa.

........................................................................................................................

........................................................................................................................

f) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia mishale. (alama 4)

Beberu hupenda wake wanaoenzi ulimbwende wao.

........................................................................................................................

........................................................................................................................

........................................................................................................................

........................................................................................................................

........................................................................................................................

g) Geuza sentensi ifuatayo iwe katika hali ya udogo wingi.

Nyoka yule mrefu alifukuzwa na watu wakubwa. (alama 3)

........................................................................................................................

........................................................................................................................

........................................................................................................................

) Eleza maana **mbili** za sentensi ifuatayo. (alama 2)

Ulezi wa mama yule ni wa manufaa.

........................................................................................................................

........................................................................................................................

Tunga sentensi **moja** inayobainisha maana ya maneno haya: (alama 2)

i) Pima
ii) Bima

........................................................................................................................

........................................................................................................................

........................................................................................................................

Unda vitenzi kutokana na maneno haya. (alama 2)

i) radhi
ii) dhalili

........................................................................................................................

........................................................................................................................

Tumia kiambishi **ki** katika sentensi kama kielezi na kama kitenzi. (alama 2)

........................................................................................................................

........................................................................................................................

for more free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or Call: 0720502479

l) Onyesha viambishi vya neno. (alama 3)
Vilivyovichukulia.

.............................................................................................................................................
.............................................................................................................................................

m) Andika upya sentensi hii kwa kufuta maagizo. (alama 2)
Kama watoto hawawathamini wavyele wao hawawezi kufanikiwa maishani.
Anza: Ni
Vigumu .....................................................................................................................................
.............................................................................................................................................

n) Tumia visawe vya maneno yaliyopigiwa mstari kuandika sentensi hii upya. (alama 3)
Ni jambo la aibu waziri mwenye taadhima kupokea chauchau

.............................................................................................................................................
.............................................................................................................................................

o) Maelezo haya yanalenga methali gani? (alama 1)
Ukiwa na mapatano ya kutenda ni kama aliyekopa. Huna budi kulitimiza.

.............................................................................................................................................
.............................................................................................................................................

p) Andika kwa kinyume (alama 1)
Aumbaye ni rabuka

.............................................................................................................................................
.............................................................................................................................................

q) Uke wa maneno haya ni : (alama 2)
i) Fahali
ii) Jogoo

.............................................................................................................................................
.............................................................................................................................................

r) Onyesha chagizo , yambwa tendwa, yambwa tendewa na kitumizi katika sentensi ifuatayo. (alama2)
Wezi walimbomolea jirani duka kwa mitaimbo Jumamosi.

.............................................................................................................................................
.............................................................................................................................................

s) Tumia alama ya kibainishi kwenye sentensi. (alama 1)

.............................................................................................................................................
.............................................................................................................................................

**4. ISIMU JAMII (alama 10)**

a) i) Eleza maana ya viziada lugha. (alama 1)

.............................................................................................................................................
.............................................................................................................................................

ii) Eleza sababu za kutumika kwa viziada lugha katika mawasiliano (alama 4)

.............................................................................................................................................
.............................................................................................................................................

b) Eleza sifa tano za sajili ya bungeni (alama 5)

.............................................................................................................................................
.............................................................................................................................................
.............................................................................................................................................

for more free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or Call: 0720502479